

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**  
**SHULE YA SEKONDARI IDODYANDOLE,**  
**S.L.P 70,**  
**ITIGI.**  
**15.12.2020**

JINA LA MWANAFUNZI.....

SHULE YA MSINGI .....

S.L.P .....

ITIGI.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IDODYANDOLE  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI, MKOA WA SINGIDA MWAKA 2021

**1. UTANGULIZI**

Nina furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Idodyandole mwaka 2021. Shule ya sekondari Idodyandole ipo umbali wa kilomita 21 kutoka manyoni mjini. Barabara ya kuelekea HEKA.

Muhula wa kwanza wa masomo 2021 unaanza tarehe 11.01.2021. hivyo unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia terehe 11.01.2021 hadi tarehe 17.01.2021 (ndani ya siku saba)

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

SARE ZA SHULE.

i. WAVULANA ni suruali ya rangi ya damu ya mzee yenyne marinda mawili iliyopindwa chini, isiyobana, viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeupe na shati jeupe lenye mikono mifupi.

ii. WASICHANA sketi ya rangi ya damu ya mzee yenyne marinda na shati jeupe la mikono mifupi. Kwa wasichana wa kiislamu wavae hijabu nyeupe na sketi ndefu yenyne rangi ya damu ya mzee na shati nusu kanzu yenyne mikono mirefu.

- SWETA la rangi ya damu yam zee kwa jinsia zote
- Sare za michezo: tisheti yenyne rangi ya bluu iliyopauka (dark blue) na truck suit yenyne rangi ya bluu.

iii. VIFAA VYA KUJIFUNZIA.

- Daftari kubwa (counter book) kumi (10) na kalamu za wino za kutosha na mkebe wa hesabu.
- Karatasi nyeupe (rimu) bunda moja kwa ajili ya kufanya mazoezi na mitihani.
- Shule ni ya kutwa hivyo mzazi jitahidi kumhudumua mwanaao kwa mahitaji ya kibinadamu kama chakula na malazi.

NB: mahitaji yote haya yatakaguliwa siku ya mwanafunzi kuripoti shulenii.

iv. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia no 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi na teknolojia yenyne dhamana ya elimu nchini na ofisi ya rais TAMISEMI yenyne jukumu la usimamizi na uendeshaji wa shule. Pia ina sharia na kanuni zinazomwongoza mwanafunzi. Hivyo mzazi unaomba kumsisitiza mwanaao kufuata sharia na kanuni za shule ambazo atapewa na kuzisoma kwa makini pindi tu afikapo shulenii.

v. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na mwanafunzi ni:  
a. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara tu utakaporipoti shulenii.

NB: TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO NA MAAGIZO NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU .

KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU

-----  
MKUU WA SHULE

0762848184

